**Masomo ya Biblia**

**kwa ajili ya**

**KANISA LA ELOHIM (COG)**

**Siku Ya Saba (7th day)**

**_________**

**Robo Ya Kwanza**

**2017**

**___________**

**KWA AJILI YA**

**Januari, Februari, Machi.**

**Kutumika na Biblia**

**___________**

**Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...**

**___________**

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**

**Jerusalem - Israel**

**-----------------------------------------------------------**

## Somo la Januari 7, 2017.

## UTHIBITISHO WA KUZALIWA UPYA

**Somo Kuu: 1 Yohana 3**

**Fungu La Kukariri: 1 Yohana 4:7, 8.**

1. Ni nini kilichosemwa kuhusu WaMasihi wa Korintho kwamba ni kweli kwetu sisi wakati huu wa sasa? 2 Wakorintho 3:2.

   **MAELEZO**: UMasihi katika hali yake ya kweli hauwezi kufichika kwa mtazamo. Ni ukweli sawia kwamba ukosefu wa UMasihi hauwezi kufichwa na muumini mwanaume au mwanamke. Sisi hatufai kutajwa tu kama WaMasihi, ni lazima tujitahidi kuwa kama jinsi hilo jina linamaanisha.
2. Ni kwa kanuni gani iliyo ya kale sisi huwa bado twapimwa nayo? Mathayo 7:20.

**MAELEZO**: Hii ni kuhusu mstari mmoja tu baadhi ya wakosoaji wa Biblia huonekana wamejifunza. Hata hivyo ni kweli kwamba tunapaswa kuzalisha matunda kwa ajili ya utukufu wake. Ni jambo baya sana kuweka madai kwa jina la mtu mwingine na kujaribu kuendelea na tabia ya huyo mtu.

3. Je, ni mambo yapi mawili yanayothibitisha mtu amezaliwa upya? 1 Yohana 5:1-3.
   **MAELEZO**: Moffatt hueleza jambo hili: "Kila mtu anayeamini kwamba Yahshua ndiye Masihi amezaliwa na Elohim; na kila mtu ambaye hupenda Baba hupenda wana waliozaliwa naye. Hivi ndivyo tuna uhakika kwamba twawapenda watoto wa Elohim, kwa kumpenda Elohim na kutii amri zake."
4. Jambo ili limesemwa vipi mahali pengine? Yohana 13:34, 35.
   **MAELEZO**: Kinyume cha hoja ambayo Masihi alitumia katika mstari wa 35, haitaonekana ya kwamba, kama upendo wa kidugu hautakuwepo baina yetu, hatutakuwa wanafunzi wake?
5. Je, ni nini hutimiza sheria? Warumi 13:1-13.
6. Jinsi gani ni lazima tujitenganishe na ulimwengu kabisa? Yohana 17:14.
7. Wakati tutajisalimisha kwa Elohim kwa ukamilifu, mwenendo wetu utakuwa upi? 1 Yohana3:9.
8. Jinsi gani tutaweza kuyafanya maisha yetu ya uMasihi kuvutia zaidi na yenye faida? 2 Wakorintho 6:14.
   **MAELEZO**: Hii bila shaka inajumuisha swali la ndoa lakini si hilo tu. WaMasihi wengi wamekwazika sana katika kazi yao ya kuhubiri, na pia katika utunzaji wa Sabato kwa sababu ya "kufungiwa pamoja isivyofaa" katika biashara.
9. Jinsi gani ingine maisha yetu yataonyesha kwamba sisi tumezaliwa tena? Wagalatia 5:24-26.
10. Katika uchambuzi wa mwisho, tutakuwa tunafanya nini? 1 Yohana3:24.

## Somo La Januari 14, 2017.

## KIASI

**Somo Kuu: 1 Petro 4.**

**Fungu La Kukariri: 1 Petro 4:7**

1. Ni kwa kiasi gani mwenye hekima alijaribu raha za dunia? Mhubiri 2:10.
2. Ni kiasi gani njia hiyo iliweza kumudu starehe ya kweli? Mhubiri 2:11; Mithali 14:12-13.
3. Ni nani hufurahishwa na starehe kama hii? Mithali 15:21.

4. Mwenye hekima alifikia hitimisho gani? Mhubiri 2:13, 14.
5. Kwa nini kuwa na kiasi hupendekezwa kuliko utovu? Mhubiri 7:2, 3.
6. Nini kinachotofautisha kati ya wenye busara na wale wapumbavu? Mhubiri 7:4.
7. Ni nini mtu mwenye hekima alimwamuru kijana kuwa makini hata katika harakati za raha? Mhubiri 11:9.
8. Ni tahadhari gani ya kuwa na kiasi imetolewa: Tito 2:2-8; Warumi 13:13; 1 Petro 1:13?
9. Je, hii inamaanisha kwamba watu wa Elohim lazima wawe wamehuzunika wakati wote? Zaburi 100:2; Isaya 12:2-3; Luka 6; 22, 23.
10. Jinsi gani MMasihi anafaa kufurahi? Wafilipi 4:4.
11. Kwa nini umakini na kuwa na kiasi ni muhimu hasa? 1 Petro 5:8.
12. Ni nini ingine twafaa kuzingatia ambayo itatuongoza tuwe na kiasi? 1 Petro 4:7.

**Somo La Januari 21, 2017.**

**KUJIFANANISHA NA ULIMWENGU**

**Somo Kuu: Waefeso 2:1-22**

**Fungu La Kukariri: Warumi 12:2**

1. Je, ni ushauri mzuri ambao ni lazima kila MMasihi anafaa kutii wakati wote? 1 Yohana 2:15-17.
2. Lengo katika maisha ya MMasihi ni lipi? Wakolosai 3:1-3
3. Ni mfano upi wa Agano la kale wa kuipenda dunia tumepewa ambao ulikuwa wa umuhimu mkubwa kwa wana wa Israeli, lakini Elohim aliulaani? Isaya 2:6-8.
4. Jinsi gani Yakobo anaeleza umuhimu wa kujitenganisha na dunia? Yakobo 1:27; 4:4-6.
5. Ni hatua gani ya mwisho Shetani alifanya kumjaribu Yahshua nyikani? Mathayo 4:8, 9.
6. Ni hamu gani ilisababisha Israeli kupotoka katika siku za Samweli? 1 Samweli 8:5-7.
7. Ni jinsi gani mawaidha ya Petro yanakubaliana na mtazamo wa kisasa kwa wanawake "huru"? 1 Petro 3:1-6. Na wanaume nao je? Mistari 7, 8.
8. Ni nini MMasihi wa kweli anafaa kuzingatia kwa wakati wote? Warumi 14:7, 21; 1Wakorintho 8:13.
9. Ni mawaidha gani mazuri, Petro anatupea ambayo tunapaswa kufikiri chochote tutafanya au popote tutaenda? 1 Petro 2:9, 10.

10. Wakati Petro alipendekeza mambo ambayo yalikuwa kinyume na mapenzi ya Elohim, Yahshua alimwambia nini? Mathayo 16:21-23.
11. Wale ambao wako na Roho Mtakatifu, watakuwa na ushirika kwa maovu? Waefeso 5:8-12.
12. Je, neema ya Elohim inatufundisha nini? Tito 2:11-13.

**Somo La Januari 28, 2017.**

**KITABU CHA UFUNUO NA MNYAMA AMBAYE JERAHA LA KIFO LIMEPONA**

**Somo Kuu: Daniel 7; Ufunuo 13:1-3.**

**Fungu La Kukariri: "Amebarikiwa anayesoma maneno ya unabii huu na wale wanaosikiliza na kuzingatia yale yaliyoandikwa humu, maana wakati umekaribia." Ufunuo 1:3.**

1. Ni kwa lengo gani na ni kwa nani Kitabu cha Ufunuo kilitolewa? Ufunuo 1:1.
2. Ni wapi ambapo mnyama amenakiliwa kwanza katika maandiko? Danieli 7:2, 7.
3. Ni nini kinatokea mara moja baada ya muda uliotolewa kwa ajili ya wanyama hawa wanne kutawala? Mstari 9, 10.
4. Je, Danieli alifadhaika kuhusu ono hili, na alifanya nini? Mistari 15, 16.
5. Malaika alitoa habari gani? Mistari 17, 18.
6. Ni mnyama gani kati ya hawa wanyama wanne Danieli alipenda kujua habari zake? Mistari 19, 20.
7. Ni kwa muda gani mrefu Danieli alimuona huyo mnyama (chini ya mamlaka ya pembe ndogo) akifanya vita na Watakatifu? Mistari 21, 22.

   **MAELEZO**: Kadiri nguvu ya mnyama wa nne itaendelea kuwa hapa na kutumia nguvu zake dhidi ya mabaki ya kweli ya watu sasa, na baadaye hadi wakati utakapofika hili tumiliki ufalme, kwa hakika kuna umuhimu mkubwa kujua huyo mnyama ni nini na yuko wapi. Ni dhidi ya huyu mnyama, basi, ujumbe wa mwisho wa onyo utapeanwa.
8. Malaika alimwambia Danieli kuwa huyo mnyama aliwakilisha nini, na pia hizo pembe zake kumi? Mistari 23, 24.
9. Jinsi gani hawa wanyama walinganishwa na wanyama wa Ufunuo? Ufunuo 13:1, 2.

   **MAELEZO**: Hebu tuchunguze kuhusu huyu mnyama. Wanyama katika Danieli walikuwa simba, dubu, chui, na mnyama mwingine bila jina. Maelezo zaidi yanasema kuwa mnyama huyu wa Ufunuo alikuwa kama chui, na miguu ya dubu, na kinywa cha simba. Hivyo basi tuna wanyama hawa watatu wa Danieli ambao wanajumuisha huyu

mnyama mmoja katika ufunuo. Lakini maelezo zaidi ni kwamba huyu mnyama wa Ufunuo pia alikuwa na vichwa saba na pembe kumi. Pia elewa ya kwamba hii ilikuwa idadi kamili ya vichwa na pembe zote za wanyama wa Danieli. Hivyo basi mnyama wa Ufunuo ni mwili kamili wa wote wale wanyama wanne. Pia utawala wa Kirumi, wa nne kutawala dunia, ulitawala sehemu zote ambazo zilitawaliwa na hawa wanyama wanne, hivyo basi ilikuwa mchanganyiko wa hao wote katika huyu mmoja.

10. Ni nini imesemwa zaidi (ukilinganisha Danieli na Ufunuo) kuhusu mnyama - kazi na nguvu ya kutesa na kiwango cha uwezo wake? Danieli 7:25 (sehemu ya mwisho) na pia Ufunuo 13:5-7.

    **MAELEZO**: Hebu sasa tulinganishe tena Danieli na ufunuo. Urefu wa wakati (miezi 42 katika mstari wa 5) kwamba mnyama wa Ufunuo angekuwa na uwezo juu ya watakatifu, pia ni sawa na "nyakati na nusu wakati" ya Danieli 7:25.
11. Ni nini kilichosemwa kuhusu mnyama huyu ambaye anatawala chini ya kichwa kimoja, kujeruhiwa kwa upanga? Alipona jeraha la kifo? Ufunuo 13:3, 12-18.

**Somo La Februari 4, 2017.**

**TOBA**

**Somo Kuu: Matendo 2:22-42.**

**Fungu La Kukariri: 2 Petro 3:9.**

1. Biblia takatifu, neno la Elohim, inatufundisha nini kuhusu toba? Ezekieli 18:31-32.
2. Je, inawezekana kuokolewa bila toba? Luka 13:1-5.
3. Ni nini ambacho ni lazima tutubu? Matendo ya Mitume 3:19; 8:20-22.
4. Je, Mtume Paulo aliye mkuu aliwaambia watu kwamba ni lazima watubu? Matendo ya Mitume 20:20, 21.
5. Petro alihubiri kuhusu toba? Matendo ya Mitume 2:38.
6. Tunapaswa kukiri dhambi zetu kwa mtu au ni kwa Elohim katika kutafuta msamaha wa dhambi zetu? Matendo ya Mitume 20:21; Warumi 14:11.
7. Ni muhimu kwa kila nafsi kutubu dhambi zake ili kuwa mwana wa Elohim? Kwa nini? Warumi 14:11, 12; Warumi 3:23; 5:12; Marko 16:16.

   **MAELEZO**: Elohim hatawamtenga watu wowote kuingia kwa ufalme kama wametubu na dhambi zao kuondolewa. Elohim hutoa msamaha kamili kwa kila mwenye dhambi wenye kutubu na kurejea kwake.

8. Mtu yeyote ambaye hajatubu dhambi zake atapata uzima wa milele? 1 Wakorintho 6:9-11; Yohana 3:3; Mithali 28: 13.
9. Yahshua alifundisha nini kuhusu toba? Mathayo 4:17; Marko 1:14, 15.
10. Ni maneno gani Yohana Mbatizaji alitumia wakati alikuwa akielezea kuhusu wazo sawa? Mathayo 3:5-8.
11. Biblia inaelezea nini kuhusu maisha ya Paulo (Sauli) kabla hajatubu? Matendo ya Mitume 9:11-18; 1 Wakorintho 15:9; Wagalatia 1:13.
12. Baada ya toba yake, maisha ya Paulo yalikuwa tofauti na yale ya awali? Matendo ya Mitume 9:20, 23-25, 29.

**Somo La Februari 11, 2017.**

## HALI YETU MBELE YA ELOHIM

**Somo Kuu: Warumi 3:10-31.**

**Fungu La Kukariri: 1 Yohana 3:2, 3.**

1. Ni kwa hali gani mtu hujipata mwenyewe? Warumi 3:9, 23.
   **MAELEZO**: Paulo, kama Myahudi, angesema ya kwamba sheria ileile inayoonyesha dhambi katika kundi moja inafanya hivyo kwa wengine pia. Machoni pa Elohim wanadamu wote huonekana kama wana unajisi na kwa hivyo damu inahitajika kusafisha, ambayo Yahshua alimwaga msalabani Kalvari.
2. Ni kutoka mstari gani wa ushahidi Paulo anaeleza ili kuthibitisha ya kwamba hukumu ni kwa ulimwengu wote? Warumi 3:10-18.
3. Lengo la sheria basi ni nini? Warumi 3:19.
   **MAELEZO**: Wakati mtu anatambua hatia yake mbele ya Elohim, ni jambo rahisi la kumwonyesha njia ya uzima. Ingewezekana kuondoa sheria, basi kuonyesha dhambi na ushawishi wa hatia kwa mamlaka ya neno la Elohim na uweza wake ingekuwa pia imeondolewa.
4. Leo, ni kundi gani ambalo Masihi hawezi kufikia? Mathayo 8:10-13.
5. Ni mfano gani mkuu unafundisha somo hili? Luka 18:11-14.
6. Dhambi ni nini machoni pa Elohim? 1 Yohana 3:4.
7. Kuibeba hatia peke yako (bila Mwokozi) huleta matokeo gani? Warumi 6:23.
   **MAELEZO**: Wale hukataa wito wa Roho Mtakatifu wa kuongoka siku moja wataibeba hatia yao pekee. Upatanisho kwa ajili ya dhambi ulitolewa kwa wote, lakini si wote watakubali msamaha wa bure kupitia damu iliyo mwagika.
8. Ni nani peke yake atauchukua mzigo wa dhambi na hatia? Isaya 53: 8, 11.

9. Ni kwa mawaidha gani yake binafsi Paulo anatusihi? 2 Wakorintho 7:1.
10. Katika Masihi, nafasi yetu mpya mbele ya Elohim ni ipi? 1 Yohana 3:1.
11. Tungali tuna tumaini hili ndani yetu, hali yetu ya kiroho inapaswa kuwa vipi tunapongojee kurudi kwake? 1 Yohana 3:2, 3. Angalia pia Daniel 12:9 na 10.

**Somo La Februari 18, 2017.**

## KUONGEZA NGUVU KWA SUMAKU YA BINADAMU KUTOKANA NA NGUVU ZA USHINDI

**Somo Kuu: Warumi 8:1-14.**

**Fungu La Kukariri: Warumi 8:28.**

1. Kuna sheria inayoongoza Roho katika utendaji wa kazi ndani ya miili yetu? Warumi 8:2.
2. Hii sheria ya Roho ya uzima itafanya nini ndani yetu kulingana na sheria? Warumi 8:2.

   **MAELEZO**: Wakati sheria hii takatifu ya Roho inaruhusiwa kufanya kazi ndani yetu, kwa asili tutazaa matunda ya Roho, na kwa hivyo tutaenenda katika kwa kutii kamili amri zote. Hivyo basi tutakuwa huru kutokana na hukumu ya sheria hii, ambayo huleta mauti.

3. Kuna mahali maalum mwilini mwa kila mtu, kwa ajili ya kuishi kwa Roho Mtakatifu? 1 Wakorintho 3:16 na pia 1 Wakorintho 6:19, 20.
4. Kama miili yetu haina nguvu ya hii Roho, na kwa hivyo kuwa najisi kwa sababu ya uwepo wa roho ovu, tamaa za kidunia, hisia, na dhambi, matokeo ni nini? 1 Wakorintho 3:17.
5. Ili sisi tupokee Roho hii, tunahitaji kufanya hatua ya kwanza, au tutasubiri Elohim kuingia ndani yetu? Yakobo 4:8-10.
6. Baba wetu wa mbinguni ako tayari kutupea uwezo kutoka juu kama vile tuko tayari kutoa chakula kwa watoto wetu wakati wako njaa? Luka 11:11-13.

   **MAELEZO**: Roho hii takatifu iliyonenwa pia kama Roho Mtakatifu, kama "wema", na "nguvu". Ni sehemu ya Baba mwenyewe, uweza kutoka mbinguni huja katika hekalu zetu na inatufanya tuwe wenye roho. Hutujaza wema, na hutujaza kwetu sifa za Mbinguni ambazo Masihi Mwokozi wetu alipambwa kimiujiza. Ni kupitia kupokea uwezo huu katika miili yetu tu, huwa tunajazwa haki.

7. Ni muhimu kwetu kuwa na njaa kwa ajili ya, na kuwa na hamu ya nguvu hii ambayo itatufanya kuwa wenye haki? Mathayo 5:6.

   **MAELEZO**: Watu wengi, kwa wakati huu, huwa na njaa na kiu ya vitu vya dunia hii, umaarufu, nafasi, pesa na anasa, ambayo yote ni ubatili, na karibuni hayo yote yatapita mbali.
8. Ni nani ambaye alifungua njia, na alitufundisha kuhusu sheria hii kwa ajili ya Roho ya uzima wa milele? Yohana 8:12.
9. Je, Mwokozi wetu ambaye alikuja kutuonyesha njia, mara kwa mara alitumia muda kukawia mbele ya baba yake, katika maombi? Luka 6:12.
10. Baada ya kukaa usiku katika maombi, ni nini ilipita kutoka kwake na kuingia katika watu ambao waliponywa? Luka 6:19.

    **MAELEZO**: Wengi wetu walicheza na sumaku wakati walikuwa watoto, au kipande cha chuma kupata nguvu kutokana na sumaku ya umeme, na kuangalia jinsi itachukua vipande vidogo vya chuma, na kuvishikilia kwa nguvu. Tunaweza kuvuta hizo kwa mara nyingi na kuiacha izivute tena na tena. Kwa muda mchache hii chuma pia itapata hizo nguvu za sumaku, mpaka itavuta vipande vidogo pia. Hii inaonyesha jinsi mtu hutumia muda wake katika maombi ya kila siku anaongezeka nguvu kutokana na nguvu na wema wa mbinguni, ambapo dhambi zatolewa kutoka miili yetu, na inakuwa hekalu kwa ajili ya Roho Mtakatifu kupata nafasi ya kuishi.
11. Baada ya Bwana kutumia muda wake katika maombi, nini kilichotokea kwa mwanamke ambaye aliliguza pindo la vazi lake? Luka 8:43-47.

## Somo La Februari 25, 2017.

## DAUDI KUTIWA MAFUTA AWE MFALME

**Somo Kuu: 1 Samweli 16**

**Fungu La Kukariri: 1 Samweli 16:13.**

1. Ni swali gani Bwana aliuuliza, wakati Samweli aliomboleza kwa ajili ya Sauli? 1Samweli 16:1.

   **MAELEZO**: Kila mtumishi wa kweli katika umri wote ana huruma. Ni moyo mwovu ufurahia juu ya yule huanguka. Paulo anasema: wale ambao wana roho wanapaswa kurejesha wale walioanguka. Wagalatia 6:1. Samweli angefanya hivyo, lakini Elohim tayari alikuwa amemkataa Sauli. Uasi wa Sauli ulikuwa wa makusudi.

2. Jinsi gani Samweli alihisi kuhusu kumtia mwingine mafuta? Jinsi gani alishauriwa ili Sauli asimshuku? Mistari 2, 3.
3. Kufika Bethlehemu, jinsi gani alionekana? Ujumbe wake ulikuwa nini? Aya 4, 5.
4. Mtazamo wa nabii Samweli wa kwanza kwa Eliabu ulikuwa upi? Mistari ya 6, 7.
   **MAELEZO**: Mipango ya kibinadamu na kazi za kudhania inadhoofisha uhai wa Kanisa leo. Mwenyezi Elohim ana mpango wa jumla kwa ajili ya mtu. Yeye anataka sisi tuingie ndani ya mpango wake, sio kujaribu kumwiingiza ndani ya mipango yetu.
5. Ni wana wangapi wa Yese walipitishwa mbele ya Samweli? Aya ya 10-12.
6. Je, Roho alishuka juu ya huyo mwana mdogo wa Yese baada kutiwa mafuta na Samweli? Mstari wa 13.
7. Ni nini ilisemwa kuhusu hali ya kiroho ya Mfalme Sauli ya baadaye? Mstari wa 14.
8. Jinsi gani Daudi aliishi "katika njia zake zote" mbele ya watu? 1 Samweli 18:14, 16.
   **MAELEZO**: Licha ya chuki yote katika moyo wa Sauli na kusudi lake kumuua Daudi likiendelea kuwa lenye nguvu, Daudi bado aliendelea kuwa shujaa na alibakia mtumishi wa kweli kwa Elohim na mfalme.
9. Wakati Sauli alifanya jaribio lake la mwisho kumuua Daudi, tukio gani la ajabu lilitokea? 1 Samweli 26: 2, 7-12.
10. Ni maombolezo gani ya huzuni Daudi alifanya juu ya Sauli na Yonathani? 2 Samweli 1:23-27.
    **MAELEZO**: "Enyi milima ya Gilboa, visiwepo juu yenu Umande wala mvua, wala mashamba ya matoleo; Maana ndipo ilipotupwa kwa aibu ngao ya shujaa, Ngao yake Sauli, pasipo kutiwa mafuta. " Mstari wa 21.

**Somo La Machi 4, 2017.**

**KUMJUA BWANA**

**Somo Kuu: Yohana 17.**

**Fungu La Kukariri: Yohana 17:3.**

1. Jinsi gani ni muhimu kumjua Bwana? Yohana 17:3.
2. Ili wanafunzi wamjue Bwana, Yahshua alifanya nini? Yohana 17:6.
3. Ni kupitia njia gani Yeye alijulisha jina lake? Yohana 17:8 (sehemu ya kwanza).
4. Ni nini ilikamilika kupitia kukubali neno lake? Yohana 17:8 (sehemu ya mwisho).
5. Je, ni hatua gani ya kwanza ili kumjua Bwana? Warumi 10:17.

6. Alipoulizwa, Petro alitangaza Yahshua kuwa nani? Mathayo 16:13-16.
7. Chanzo cha ufunuo wa Petro kilitoka wapi? Mathayo 16:17.
8. Kwa nini ufunuo utokao kwa Elohim unahitajika ili kumjua Yahshua? 1 Wakorintho 15:45-50.
9. Ni wapi Yahshua alisema ya kwamba ametoka? Yohana 6:38; Yohana 17:5.
10. Mtazamo wa Wayahudi kuhusu madai hayo ulikuwa upi, na ni nani ambaye waliamini kuwa baba yake? Yohana 6:41, 42.
11. Jinsi gani Paulo anasema tunapaswa kumjua Masihi? 2 Wakorintho 5:16-21; Wakolosai 1:13-20; Waebrania 1:1-3.

    **MAELEZO**: Ingekuwa vizuri kwa ajili yetu, kama tukijifunza maandiko kama vile 1Yohana 2:4-6, na 1 Yohana 1:3-7, na pia sura ya 3 ya 1 Yohana. Inaonekana sasa kwa nini kuna uzima wa milele kwa kumkubali Yahshua, ndani yake unakaa utimilifu wote wa Elohim. Tukiwa na Yahshua kwa namna hii, anatumiliki na ndani yetu tuna utimilifu wa Mbinguni. Wakolosai 1:26, 27.

**Somo La Machi 11, 2017.**

**KUNDI NDOGO**

**Somo Kuu: Ezekieli 34.**

**Fungu La Kukariri: Ezekieli 34:31.**

1. Je, ni neno gani Mwokozi alitumia kuonyesha Kanisa lake? Luka 12:32 (sehemu ya kwanza).
2. Je, uhusiano wa Mwokozi kwa kundi hili ni upi? Mika 4:8 (sehemu ya kwanza).
3. Bwana ameahidi nini kwa kundi hili? Luka 12:32 (sehemu ya mwisho); Mika 4:8 (seh emu ya mwisho).
4. Ni malalamiko gani Bwana alikuwa nayo juu ya wachungaji wa kale? Ezekieli 34:3, 4
5. Kama matokeo ya kuachanishwa, ni nini kilichotokea kwa kundi hilo? Ezekieli 34:5, 6
6. Mtazamo wa Elohim kwa wachungaji hao ulikuwa upi? Ezekieli 34: 10.
7. Aliahidi kufanya nini kwa ajili ya kundi lake lililotawanyika? Ezekieli 34:12-15.
8. Wale wachungaji wa kale walilisha kundi la kondoo na nini? Ezekieli 34:18, 19

    **MAELEZO**: Hii inahusu makuhani na manabii ambao walificha ukweli kwa watu katika siku zao.
9. Wachungaji walifanya nini ili kutawanya kundi la kondoo? Ezekieli 34:21.

10. Jinsi gani Bwana alikabiliana na hali hii? Ezekieli 34:23, 24.
11. Ni ahadi gani Elohim alifanya nao na ni baraka gani zitafuata? Ezekieli 34:25, 26
12. Je, ni ahadi gani zingine watatimiziwa? Ezekieli 34: 27, 28.
13. Ni nini zaidi itafanywa kwa ajili yao? Ezekieli 34: 29.
14. Hatimaye wao watajua nini? Ezekieli 34: 30, 31.

**Somo La Machi 18, 2017.**

**NAKALA ZA MBINGUNI KITABU CHA UZIMA CHA MWANA-KONDOO**

**Somo Kuu: Ufunuo 3.**

**Fungu La Kukariri**: "Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake." **mstari 5.**

1. Kuna kitabu ambacho kimepangwa mbinguni kwa ajili ya kumbukumbu za watu wanaoishi katika dunia hii? Malaki 3:16.
2. Ni nini imesemwa kuhusu ukombozi wa wale ambao majina yao yatapatikana katika kitabu cha uzima? Malaki 3:17; pia Daniel 12:1.
3. Ni faida gani juu ya waumini, kujua majina yao yameandikwa mbinguni? Luka 10:19, 20.
4. Kuna vitabu vingine vitafunguliwa licha ya Kitabu cha uzima wakati wa hukumu? Ufunuo 20:12
5. Baada ya watu kujumuishwa katika familia ya mbinguni, na majina yao yameandikwa katika Kitabu cha uzima, na kuendelea katika haki, Je, inawezekana kwa majina yao kutokuwa siku ya hukumu? Ufunuo 3:5.
6. Baada Paulo kuhubiri injili, na kweli alikuwa mmoja wa familia hii takatifu, yeye alisema nini kuhusu hatari ya kukataliwa? 1 Wakorintho 9:27.
7. Tumeaambiwa nini zaidi kuhusu hatari ya kuanguka, baada ya kupokea na kukionja kipawa cha Roho Mtakatifu? Waebrania 6:4-8; 1 Wakorintho 10:12.
8. Ni nini itakuwa matokeo kwa mtu ambaye aliishi maisha yake katika dhambi na kuishi kwa haki katika siku zake za mwisho, au wakati mtu mwenye haki atapotoka? Ezekieli 33: 12, 15-19.
9. Hatima ya wale ambao majina yao hayatapatikana katika Kitabu cha uzima cha Mwanakondoo itakuwa ipi? Ufunuo 20:15; pia: 21 27.

10. Ni nini kitatendeka kwa mnyama, na pia wale huabudu mnyama, wakati vitabu vya mbingunini vitafunguliwa? Danieli 7:9-11; Ufunuo 14:9, 10; pia Ufunuo 20:13-15.

**KITABU CHA UKUMBUSHO**

“... Ndipo wale waliomcha Bwana waliposemezana wao kwa wao. Naye Bwana akasikiliza, akasikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele zake, kwa ajili ya hao waliomcha Bwana, na kulitafakari jina lake. Nao watakuwa wangu, asema Bwana wa majeshi, katika siku ile niifanyayo; naam, watakuwa hazina yangu hasa; nami nitawaachilia, kama vile mtu amwachiliavyo mwanawe mwenyewe amtumikiaye." Malaki 3:16, 17

**Somo la Machi 25, 2017.**

**KUJILINDA DHIDI YA UGOMVI NA UDANGANYIFU**

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 3.**

**Fungu La Kukariri: Warumi 16:17.**

1. Kuna hatari yoyote ya kudanganywa? Wakolosai 2:8; 1 Yohana 4:1.
2. Ni nini itatendeka kwa wale hufuata mafundisho ya mtu? Wakolosai 2:20-22.
3. Je, wanafunzi waliielewa injili au ujumbe wa Masihi kwa mara ya kwanza? Luka 9:51-56.
4. Hata baada ya Pentekoste jinsi gani Petro alishindwa katika kuongoza Kanisa? Wagalatia 2:11-13.
5. Ni kwa njia gani watu udanganywa kwa urahisi? 2 Petro 2:1-3.
6. Ni hali gani mbaya iliyotokea Korintho ambayo inaweza kuwa ndiyo ilileta matokeo ya udanganyifu? 1 Wakorintho 1:11-13.
7. Ni nini baadhi ya waumini walijaribu kuleta ndani ya Kanisa katika wakati wa Paulo? Wagalatia 4:8-11; Matendo ya Mitume 15:5.
8. Ni kwa maneno yapi yenye nguvu Paulo alitumia kukabiliana na mafundisho haya? Matendo 15: 10.
9. Ni mwenendo gani wa sasa ulizuia hata Kanisa la kwanza? 2 Yohana 9, 10.
10. Jinsi gani Yohana aliwaonya WaMasihi kuhusu wadanganyifu katika siku zake? 2 Yohana 6, 7.
11. MMasihi atalazimika kufanya nini ili kujua ukweli na kukosa kudanganywa? 1 Yohana 4:1.

**MAELEZO**: Wale wanaodanganywa kwa hiari yao wanaweza kugawanywa katika makundi mawili. Kuna wale wanaopenda maagizo ya wanadamu hivyo vizuri kwamba huwa wanakataa kukubali ushahidi kutoka kwenye Biblia — neno takatifu la Elohim linaweza kuvuruga mawazo yao sasa. Pia kuna wale ambao hawana nia ya kutosha katika ukweli ili kujifunza wenyewe.

12. Jinsi gani Yahshua alitoa onyo kuhusu wadanganyifu katika siku hizi za mwisho? Mathayo 24:4, 5, 11, 24.
13. Jinsi gani tunapaswa kuzijaribu roho? Isaya 8:20.
14. Ni juu ya msingi gani tutalazimika kujenga ili tuwe na hakika ya kutodanganywa? Waefeso 2:20-22 Wagalatia 1:8; 2 Wakorintho 13:1; Warumi 3:4.
15. Baadhi ya wachungaji wataonyesha kutokuwa na hiari kiasi gani ya kukubali ukweli wa neno la Elohim takatifu? Ezekieli 22:26-31.